



وَعَدَ اللَّهُ الَّذِينَ مَأْمَنُوا مِنْكُمْ وَعَمِلُوا الصَّالِحَاتِ لَيَسْتَخْفَتُنَّهُمْ فِي الْأَرْضِ كَمَا أَفْتَخَفَ
الَّذِينَ مِنْ قَبْلِهِمْ وَلَمْ يُنْكِنُوهُمْ دِينُهُمُ الَّذِي أَنْهَى مُلْكَهُمْ وَلَمْ يُنْكِنُوهُمْ مِنْ بَعْدِ خَوْفِهِمْ إِنَّمَا
يُعْذِّبُونَهُمْ لَا يُشْرِكُونَ بِهِ شَيْئًا وَمَنْ كَفَرَ بِهَذَا ذَلِكَ فَأُولَئِكَ هُمُ الظَّالِمُونَ

Toleo: 03 / 1446 H

Jumatatu, 30 Muharram 1446 H

05/08/2024 M

Taarifa kwa Vyombo vya Habari

Kama Umma Mmoja: Tunamshukuru Mwenyezi Mungu kwa Kuangamizwa kwa Dhalimu Hasina
na Tunawaombea Kuporomoka Madhalimu Wote Wanaoukandamiza Ummah

(Imetafsiriwa)

Baada ya majuma kadhaa ya ukandamizaji wa kikatili dhidi ya watu wa Bangladesh na dhalimu Hasina, genge la serikali yake, na wachungaji wake wa kigeni, alilazimishwa kidhalilifu kuikimbia nchi. Waislamu shupavu wa Bangladesh, wakiongozwa na wanafunzi jasiri, walivumilia ukatili usio na kifani na hatimaye kulazimisha kuondolewa kwake kuitia wimbi lisilozuulika la maandamano ambayo yalimshinda dikteta huyo.

Waislamu wa Bangladesh kwa mara nyingine tena wameangazia uwezo mkubwa ndani ya ummah, wakionyesha hatima isiyopukika inayowangojea madhalimu wanaowafanya ukatili raia wao. Ingawa huu ni ushindi wa aina yake, ummah lazima uzingatie mafunzo ya matukio kama hayo katika nchi kama Misri na Sudan. Misimamo ya kikoloni inaenea ndani kabisa ya rasilimali za ummah, ikinyakua kwa ujanja ushindi kwa kuwatupilia mbali madhalimu vibaraka wao pindi kufaa kwao kunapokwisha, ila kuwabadihisha tu kwa watu ambaa uaminifu wao unabakia mapajani mwa dola za kigeni na zeny uadui.

Umma lazima uhakikishe kwamba rasilimali zake, kama vile majeshi, zinabakia chini ya udhibiti wake ili kwamba matakwa ya uadilifu wa kweli kwa wote—yanayojumuishwa tu ndani ya mfumo ulioteremshwa na Mwenyezi Mungu (swt)—yaweeze kuasiwi kwa uhuru kamili na umma wa Muhammad (saw).

Tunawapongeza Waislamu wa Bangladesh kwa subira na ustahimilivu wao, na tunaomba dua kwamba Mwenyezi Mungu (swt) awakubali mashahidi wengi na huu uwe ndio mwanzo wa mwamko mkubwa kwa Waislamu wa Bangladesh katika kusimamisha rehma na uadilifu wa Uislamu kwa watu wote.

[وَلَا تَحْسِنَ اللَّهُ غَافِلًا عَمَّا يَعْمَلُ الظَّالِمُونَ إِنَّمَا يُؤَجِّرُهُمْ لِيَوْمٍ شَنْخَصُ فِيهِ الْأَبْصَارُ]

“Wala usidhani Mwenyezi Mungu ameghafilika na wanayo yafanya madhaalimu. Hakika Yeye anawaakhirisha tu mpaka siku yatapo kodoka macho yao.” [Quran 14:42]

Afisi ya Habari ya Hizb ut Tahrir
Australia

Tovuti Rasmi ya Hizb ut Tahrir:

Tovuti: www.hizb-ut-tahrir.dk

Pepe: info@hizb-ut-tahrir.dk

www.hizb-ut-tahrir.org

Tovuti ya Afisi Kuu ya Habari ya Hizb ut Tahrir:

www.hizb-ut-tahrir.info